**Learning by Ear**

**"Everyone's Different – Respect for Minorities"**

**Episode 04**

**Title: "Pink City" – Gays in Cape Town**

**Author:** Kerstin Poppendieck

**Editor:** Katrin Ogunsade

**Proofreading/Translation:** Tony Dunham

<u>List of Characters:</u>

| | | | |
|---|---|---|---|
| ***Narrator*** | female | about 30 | english |
| ***Ryan*** | male | about 22 | english |
| ***Junior*** | male | 23 | english |
| ***Leonie*** | female | about 25 | english |

**INTRO:**

Karibu kwenye sehemu ya nne ya kipindi chetu "**Kila mtu ni tofauti-Kuzingatia maslahi ya jamii za watu walio wachache**". Kipindi hiki kinahusu watu ambao hubaguliwa kwa sababu kadha wa kadha. Hata hivyo watu hao hutetea haki zao na pia kuwa na mazingira yasiyokuwa na ubaguzi. Leo tunakutana na vijana wawili kutoka Afrika Kusini. Ryan na Junior wana sifa fulani za kufanana: wote wanaishi Cape Town, ni marika na wote ni mashoga. Hata hivyo, maisha yao hayalingani: Ryan ni raia wa Kizungu wa Afrika Kusini, Junior ni raia mweusi wa Kongo aliyekimbilia Afrika Kusini. Taifa la Afrika Kusini lina sifa za kipekee barani Afrika kwa kuridhia watu wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja. Tuandamane tukawatembelee vijana hao wawili mjini Cape Town hivi leo.

1. **O-Ton Ryan**

*Hamjambo. Jina langu ni Ryan. Mimi ndiye nitakayewahudumia hivi leo. Orodha ya vyakula ndio hii hapa. Chagueni mtakacho. Nitakuja hivi punde.*

2. **SFX: Beefcakes**

3. **Narrator**

Ryan anafanya kazi kwenye mgahawa wa watu wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja mjini Cape Town. Kila pahali kuna rangi ya waridi: Wahudumu huvaa fulana za rangi ya waridi na nyeusi, mashada ya maua ya rangi ya waridi yameangikwa ukutani na kwenye viti kumewekwa kofia za rangi ya waridi. Ryan pia amevaa shada la maua shingoni na dangarizi. Mavazi hayo si ya kawaida kama huko mgahawa wa Beefcakes ulivyo. Wahudumu wote wa mgahawa huo ni watu wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja. Ryan pia ni mmoja wao. Bwana huyo anapenda hali ya maisha ya Cape Town.

**4. O-Ton Ryan**

*Napenda hali hapa mjini. Nafurahi sana kwa kuwa kila mtu hapa na hamsini zake. Si sana mtu kubughudiwa. Unaweza kuishi utakavyo. Hakuna chuki. Pengine kuna chuki kidogo lakini hakuna anayenishughulikia pindi nikiamua kutembea barabarani nikiwa na mavazi yangu ya rangi ya waridi.*

**5. Narrator**

Junior alitaka sana kuja Cape Town kwa sababu hizo hizo alizozitaja Ryan.

**6. O-Ton Junior**

*Jina langu ni Junior. Nina umri wa miaka ishirini na mitatu (23). Ninatoka Kinshasha katika Jamhuri ya Kidemokrasia ya Kongo.*

***7. SFX: Door-Buzzer***

**8. Narrator:**

Junior yumo katika ofisi ya Shirika la Passop. Mara nyingine hufanya kazi ya kujitolea katika ofisi hiyo. Shirika hilo la Passop ni shirika linalowasaidia wakimbizi wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja. Kijana huyo mkongo amekuwa akiishi Cape Town kwa muda wa mwaka mmoja kufikia sasa.

**9. *O-Ton Junior***

*Nilikuja Afrika Kusini kwa kuwa nilitaka uhuru. Nisingeweza kupata uhuru nchini Kongo- Kinshasa. Nilikuwa na wasiwasi kila mara. Nilikuwa katika chuo kikuu lakini sikuweza kuendelea na masomo kwa sababu ya ubaguzi. Raia wa Kongo ni wahafidhina. Vigumu sana kwa mtu kama mimi kukubalika na familia yangu na jamii kwa jumla. Kwa hivyo nikatafuta nchi ambayo ingeniruhusu kuishi nipendavyo. Sikufanikiwa kwenda Ulaya au Marekani. Nilikuja Afrika Kusini kwa sifa zake za uhuru wa watu kama mimi.*

**10. Narrator**

Junior ni miongoni mwa maelfu ya wakimbizi wa Kiafrika wanaokuja Afrika Kusini kukimbia dhuluma wanazotendewa kwa kushiriki mapenzi ya jinsia moja. Serikali ya Afrika Kusini imewapa hadhi ya ukimbizi. Kulingana na takwimu za Passop, nchi thelathini na nane miongoni mwa nchi hamsini na sita barani Afrika zina sheria zinazoharamisha uhusiano wa kimapenzi kwa watu wa jinsia moja. Katika baadhi ya hizo nchi mtu anaweza kufungwa gerezani kwa muda usiozidi miaka kumi na mitano (15). Junior alikuwa akibughudhiwa mara kwa mara nchini Kongo. Maisha yalikuwa magumu hasa alipokuwa akisoma mjini Kinshasha.

***11. O-Ton Junior***

*Maisha yalikuwa magumu. Daima nilikuwa peke yangu. Kulikuwa na watu wengine wengi kama mimi katika chuo kikuu lakini tusingethubutu kukutana. Ilikuwa hatari. Tulijifanya kwamba hatukuwa tukishiriki mapenzi ya jinsia moja wala hatukutaka watu wazijue hali zetu. Nilikuwa nikosomea sheria na hata wahadhiri walinishambulia wakiniambia kwamba sikuwa na akili timamu. Mama yangu mwenyewe alitaka kuniua. Kwa hivyo, nikajiamulia "Nitakwenda zangu. Siwezi kuishi hapa".*

***12. SFX: Straße Kapstadt***

**13. Narrator**

Junior anatembea katika barabara za mji wa Cape Town. Amevaa suruali inayombana aina ya Jeans na koti jeusi. Amejipaka wanja na pia rangi ya midomo. Asingefanya hivyo nchini Kongo. Mji wa Cape Town unachukuliwa kuwa mji bora zaidi kwa wapenzi wa jinsia moja barani Afrika. Kuna matamasha ya muziki, vilabu na migahawa maalumu kwa watu wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja. Mji huo lakabu yake ni Pink City maanake Jiji la Waridi. Hata hivyo, Junior anauelewa mji huo kwa namna tofauti.

***14. O-Ton Junior***

*Mji wa Cape Town ni mzuri kwa watu kama sisi iwapo utaishi katika sehemu salama. Wazungu wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja wana uhuru zaidi. Na ni hao hao wazungu wa Afrika Kusini wanaotangaza hali zao za kimapenzi na pia kuhamasishana kuhusu mapenzi ya jinsia moja. Watu wanaoishi kwenye mitaa ya watu weusi hawaridhii mambo hayo. Hali ni ngumu sana katika maeneo hayo.*

***15. SFX: Restaurant Beefcakes***

**16. Narrator**

Suala la mapenzi ya jinsia moja linahusishwa pia na rangi za wahusika. Wazungu wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja wana uhuru wa kuishi watakavyo katika Jiji la Cape Town. Hali ni tofauti kwa mtu mweusi. Mara nyingi wanawake weusi wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja hubakwa. Baadhi ya watu wana itikadi kwamba mwanamke msagaji akibakwa huondokana na maisha hayo ya usagaji na akaishia kupenda mpenzi wa kiume badala ya kupendana na wanawake wenzake. Lakini Ryan,ambaye

ni mzungu, hajakumbana na visa vingi vya bughudha katika mgahawa anaofanyia kazi.

17. ***O-Ton Ryan: Problems at Beefcakes***

*Mara kwa mara, utapata wapumbavu wanaofurahia kututania. Lakini hilo ni jambo la nadra sana. Na tunavyoishi hapa utadhani ni familia moja. Mtu anapomkejeli mhudumu yeyote hapa, wahudumu wengine kiasi watano huja mara moja na kumkabili huyo mtu.*

18. ***SFX: Strandpromenade***

19. **Narrator**

Leonie anashangazwa na hiyo tabia ya kuwabagua wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja. Bibi huyu wa Cape Town si mmoja wa hao wapenda mapenzi ya jinsia moja. Anapenda kukaa mwambaoni na kuwatazama watu wakiendelea na harakati zao za maisha. Anaridhia jinsi watu walivyo tofauti, wanavyoishi, wanavyovaa na wanavyozungumza. Marafiki zake wengi ni watu wanaochangamkia mapenzi ya jinsia moja. Leonie haoni sababu ya mtu kumbagua mwenzake kwa kuwa shoga au msagaji.

20. ***O-Ton Leonie***

*Kusema kweli hawana tofauti na marafiki zangu wengine. Tunafurahia mambo sawa. Mimi sikai nao ati kwa sababu wanapenda mapenzi ya jinsia moja. Urafiki hauna cha ushoga au usagaji. Urafiki unategemea mtu binafsi. Ninazingatia zaidi kwamba tunafurahia mambo sawa, tunafurahia kuwa pamoja, tunaandama maadili ya kufanana na tunaweza kwenda likizoni pamoja. Urafiki wao hauna tofauti na wa wale walio na wapenzi wa jinsia tofauti.*

KW Anfang

***21. SFX: Strandpromenade kurz hochziehen***

**22. Narrator**

Leonie anatazama wanaume wawili walioshikana mikono wanaotembea huku wakicheka.

***23. O-Ton Leonie***

*Ni kawaida kwao kushikana mikono hadharani. Wanaridhia maisha yao ya kupenda watu wa jinsia sawa na yao. Sidhani kuna shida kwao kudhihirisha mapenzi yao hadharani. Watu hao wawili wanapendana na wanahisi vizuri.*

***KW Ende***

***24. SFX: Strandpromenade kurz hochziehen***

***25. O-Ton Leonie***

*Haya si mambo ya kuridhiwa vivi hivi. Kuna watu chungu nzima ambao wanatilia maanani sana mitizamo ya watu kuhusu mapenzi. Watu hawa wanaoshiriki mapenzi ya jinsia moja hawawezi kubadilika wala haina maana kwamba utu wao una kasoro kwa sababu hiyo. Ninaamini kuwa lau watu wengi wangehamasishwa tangu wakiwa wadogo, kusingekuwa na ubaguzi dhidi ya watu hawa.*

**26. Narrator**

Junior ambaye ni Mkongo anaamini hivyo. Anasikitika sana kwamba hali jijini Cape Town si kama alivyotarajia. Hajapata ajira na mara nyingi hana pesa. Hata hivyo, hajakata tamaa. Anajitahidi jinsi wafanyavyo watetezi wa

wapenzi wa jinsia moja kote duniani.

***27. O-Ton Junior***

*Haya mambo ya wapenzi wa jinsia moja si hapa tu Afrika Kusini au Kongo. Wanapatikana kote duniani na wanajitahidi kutetea haki zao. Baadhi ya viongozi wa Kiafrika wanasema hali hii si tabia ya Kiafrika. Hayo si kweli. Mimi sikulazimishwa kuwa hivi nilivyo. Hakuna aliyenifundisha. Ndivyo nilivyo. Kuna Waafrika weusi chungu nzima ambao ni kama mimi. Katika kila nchi. Ni jambo la wazi mbona.*

**28. Narrator**

Ryan, ambaye ni mhudumu wa mgahawa wa Beefcakes anatumai kwamba siku za usoni watu hawatazingatia mitazamo ya wenzao kwenye suala la mapenzi.

***29. O-Ton Ryan***

*Chuki na uhasama si sifa za ulimwengu bora. Watu wana tabia ya uonevu. Laiti watu kama sisi tungekuwa na uhuru wa kutembea kila pahali bila kubughudhiwa au kukejeliwa. Naamini tunahitaji subira na yamkini mambo yakatengemaa siku za usoni.*

***30. Outro:***

Wito huo wa Junior na Ryan kutoka jiji la Cape Town wakiwahimiza binadamu kuvumiliana, ndio unaotukamilishia sehemu hii ya kipindi chetu cha **Noa Bongo Jenga Maisha Yako**. Je, wewe umeshawahi kukumbana na visa vya ubaguzi? Au umeshawahi kuwabagua wengine? Tuandikie ujumbe utupashe yaliyojiri. Ukitaka kusikiliza tena sehemu hii au sehemu nyingine za kipindi chetu, fungua wavuti wetu www.dw.de/lbe. Kwaheri

kwa sasa!